

Simba na ng'ombe dume watatu

— Hadithi kutoka Somalia



Hapo zamani za kale palikuwa na msitu mkubwa na mzuri nchini Somalia. Katikati ya msitu, katika miti mirefu, kulikuwa na kijani kibichi, tambarare na mto unaotiririka.

Hapo palikuwa panaishi ng'ombe dume watatu, ng'ombe dume mweupe, ng'ombe dume mweusi na ng'ombe dume wa kahawia. Walikuwa marafiki wakubwa na waliishi vizuri pamoja.

Det var en gang en stor og fin skog i Somalia. Midt i skogen, mellom de høyreiste trærne, lå det en grønn, vid slette, med en elv som rant igjennom. Der bodde det tre okser; en hvit okse, en svart okse og en brun okse. De var bestevenner og levde fint sammen.



Siku moja walitembelewa na simba. Ng'ombe watatu waliogopa sana, walikusanyika pamoja na kujiandaa kupigana na simba. Kwa maana ingawa simba alikuwa na nguvu kuliko wao, wakikusanyika pamoja watakuwa wenye nguvu kuliko yeye!

En dag fikk de besøk av en løve. De tre oksene ble *så* redde at de samlet seg sammen og gjorde seg klar til å sloss med løven. For selv om løven var sterk, var de *sammen*, sterkere enn ham!



“Tulieni mimi si hatari”, alisema simba na kulala chini kwa miguu yake yote minne.

"Unaona, ninaishi upande wa pili wa msitu, kule ni upweke sana na ukiwa. Je! Hatuwezi kuishi hapa pamoja, kuwa marafiki na kutunzana kila mmoja wetu. Ng'ombe walidhani ni wazo nzuri kuwa na simba kama rafiki, ambaye angeweza kuwalinda dhidi ya wanyama wakali.

«slapp av, jeg er ikke farlig», sa løven og la seg ned på alle fire. «dere skjønner, jeg bor på den andre siden av skogen, og der er det så ensomt og øde. Kan vi ikke bo her sammen, være venner og passe på hverandre.» Oksene syntes det var en god idé å ha en løve som venn, en som kunne beskytte dem mot de farlige dyrene der ute.



Siku moja mchana ng'ombe mweupe alikuwa nje ya zizi akila majani, wakati wale wengine wawili wakiwa wamelaa. Kisha simba akawaenda wale ng'ombe wawili na kuwanong'oneza polepole masikioni mwao: "Unajua nini? Ng'ombe mweupe ni mweupe sana na wakati wa jioni rangi yake huangaza sana. Wanyama hatari huko nje watamtambua kwa urahisi na pia kuweza kuja hapa na kutula sisi wote, hebu tumfukuzeni ng'ombe mweupe mbali"

En dag var den hvite oxen ute på beite, mens de to andre tok seg en ettermiddagslur. Da gikk løven bort til de to oksene og forsiktig hvisket i ørene deres: «Vet dere hva? Den hvite oxen er så lys at han skinner skarpt om kvelden. De farlige dyrene der ute vil lett legge merke til ham også komme hit og spise oss alle sammen, la oss jage den hvite oxen vekk».



Wale ng'ombe wawili waliposikia hivyo, waliogopa sana. “Simba yupo sahihi” walisema na kumfukuza mbali ng'ombe mweupe.

Da de to oksene hørte dette, ble e veldig redde. «Løven har rett» sa de og jaget vekk den hvite oxen».



Baada ya kumaliza kumfukuza ng'ombe mweupe, haikuchukua muda sana kabla ya simba kumpata ng'ombe mweupe akiwa peke yake katika kingo za mto, alimkamata na kumla.

Det tok ikke lang tid før løven fant den hvite oxen alene ved elvebredden og spiste han opp.



Baada ya muda simba alimuendea yule ng'ombe wa rangi ya kahawia na kumnong'oneza sikioni: "Unajua nini, ng'ombe mweusi ni mweusi sana wakati wa mwanga wa mchana anaonekana vizuri sana. Wanyama hatari huko nje watamtambua kwa urahisi na pia kuweza kuja hapa na kutula sisi wote, hebu tumfukuze mbali"

Etter en stund gikk løven bort til den brune oxen og hvisket i øret hans: <<Du vet du hva, den svarte oxen er så mørk at han synes så godt i dagslyset. Alle de farlige dyrene der ute kommer til å legge merke til ham. Også kommer de hit og spiser oss opp alle sammen. La oss jage han bort>>.



Yule ng'ombe wa kahawia aliposikia hivyo, aliogopa sana. "Tumfukuze mbali" alisema simba. Ng'ombe wa kahawia akaungana nae kumfukuza ng'ombe mweusi.

Da den brune oxen hørte dette, ble han kjempe redd. «La oss jage ham bort sa løven». Dette gikk den brune oxen med på.



Baada yakumaliza kumfukuza ng'ombe mweusi, haikuchukua muda sana kabla ya simba kumpata ng'ombe mweusi akiwa pekee yake, alimkamata na kumla. Alirudi nyumbani alipokuwepo ng'ombe wa kahawia na kujifanya hajui kitu chochote kilichotokea.

Det tok ikke lang tid før løven fant den sorte oxen alene, fanget ham og spiste ham. Også dro han tilbake og latet som ingenting.



Sasa ikawa amebakia ng'ombe wa kahawia na simba pekee yao. Ilikuwa zamu yake kuliwa na simba.

Nå var den brune oxen alene igjen med løven.
Og det var hans tur bli spist opp.



Simba alimwinda na kumkamata yule ng'ombe wa kahawia. Ng'ombe wa kahawia alipigana alivyoweza, lakini bila marafiki zake hakuwa na nguvu za kutosha kupigana na simba. Simba alitoa kucha na meno yake makali na akamng'ata yule ng'ombe akafa.

Løven jaget og fanget den brune oxen, og oxen sloss tilbake alt han kunne. Men uten sine venner var han ikke sterk nok til å kunne sloss med løven. Løven tok frem de skarpe klørne og tennene og bet oxen i hjel.



Wakati ng'ombe wa kahawia akivuta pumzi yake ya mwisho, alisema:

“Si leo ndio nakufa, bali toka siku ile nilipowafukuza marafiki zangu”.

I det den brune oxen tok sitt aller siste åndedrag, sa han:

<<Det er ikke i dag jeg døde, men den dagen jeg jagde bort min venn.>>





Illustratør: Svetlana Voronkova

Se flere fortellinger på morsmal.no